SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.23 NO. 2 2024
DOI: 10.51984/JOHS.V23I2.3141

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: http://www.sebhau.edu.ly/journal/johs

# Ufeministi Unavyopingana Na Uislamu Kuhusu Mwanamke

Jabir Alzarok Jabir

Department of Languages and African Studies, Faculty of Arts, Sebha University, Libya

**Keywords**
Ufeministi
Kiislamu
Mwanamke
Jamii
Uislamu Mtume

**ABSTRACT**

Makala imejadili namna Nadharia ya Ufeministi inavyopingana na dini ya Uislamu juu ya nafasi ya mwanamke. Aidha makala imebainisha baadhi ya aya za Kurani tukufu na hadithi za Mtume Muhammad SAW zinazodaiwa kuendeleza unyanyasaji na ukandamizwaji wa mwanamke. Ukandamizwaji wa mwanamke hasa katika kipengele cha dini na ndoa umekua ukijadiliwa na kuzua migongano ya kihakiki. Suala la umiliki wa mali limeonekana kwa kiasi kikubwa kumtenga mwanamke kiuchumi. Nadharia wa Mkabala wa Kiisilamu na Nadharia ya Ufeministi imetumika katika kujadili hoja za wana Ufeministi wa Kimagharbi kuhusiana na suala ukandamizwaji wa mwanamke. Hivyo, makala inaazimia kufuta fikra zilizo zoeleka kuwa, kinachotendeka katika nchi za magharibi ni kigezo cha taaluma na maisha bora ya ulimwengu.

# النظرية النسوية وتعارضها مع الإسلام بخصوص المرأة

جابر الزروق جابر

قسم اللغات والدراسات الأفريقية، كلية الآداب، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
المرأة
الإسلام
المجتمع
النظرية النسوية
الرسول (صلى الله عليه وسلم)

**الملخص:**

هدة المقال تهدف لتوضيع النظرية النسوية وتعارضها مع الإسلام بخصوص المرأة ،وذلك من خلال الاستشهاد ببعض الآيات القرآنية و الاحاديث النبوية التي تنبذ الإساءة والقمع ولاضطهاد ضد المرأة ،وكذلك يتناول قضية المرأة في جوانب الدنية و الاجتماعية و الاقتصادية وتحث المقال على التوحيه والتأكيد على مراجعة النظرية النسوية والمقالات الأدبية والبحث فها والتخلي عن الأفكار الغربية التي تتعارض مع الإسلام.

## 1.0. Utangulizi

Nadharia ya Ufeministi inatokana na harakati za kumkomboa mwanamke dhidi ya uonevu unaotokana na taasubi za kiutamaduni zinazomkandamiza. Asasi za dini, ndoa na elimu kwa kiasi kikubwa zinashambuliwa na wanaharakati wa nadharia hii. Katika makala hii dhana ya Ufeministi imetumika kwa tafsiri ya "Feminism". Harakati za waitifaki wa nadharia hii mwanzoni zilipingwa vikali hasa kiitikadi. Hata hivyo baadaye ikapata ushawishi mkubwa na kuwa nadharia maarufu katika kuhakiki na kutafiti kazi za fasihi. Aidha nadharia ya Ufeministi wa Kiislamu imekuwa ikitumiwa na baadhi ya wahakiki na watafiti katika taaluma ya fasihi. Kwa upande mwengine nadharia hii imeathiri falsafa ya baadhi ya wasanii. Nadharia ya Ufeministi imezua matapo tofauti. Kuna matapo yalioyotokana na mazingira na yale yanayotoka na itikadi. Tutapitia kwa sehemu kadri tunavyoendelea na makala hii.

### 1.1 Tatizo la Utafiti

Wimbi la madai ya wanawake kutaka haki sawa na wanaume na uhuru wa kujiamulia kazi na mtindo wa maisha wanayotaka kama katika jamii za Kimagharibi limeanza kubisha hodi katika jamii mbalimbali za wanawake Waisilamu. Hata hivyo, mapambano dhidi ya ukandamizwaji wa uana halijapokelewa vema miongoni jamii za Waisilamu kutokana na dhana kuwa harakati hizo zinatoka Magharibi na isitoshe kila jamii ina tajriba ya maisha yake. Aidha, Ingawa wanaharakati wa Ufeministi wa Kimagharibi wanaamini kuwa wanawake kote ulimwenguni wanakabiliwa na mikandamizo ya wanaume duniani kote. Hata hivyo, ukweli ni kwamba wanawake hutofautiana kimatatizo. Asasi za kiutamaduni hutofautiana kati ya jamii moja na nyingine kutokana na mila, desturi na itikadi zinazoongoza maisha ya jamii husika. Hivyo basi makala hii ina azma yakuondosha fikra potofu za wanafeminsiti wa Kimagharibi dhidi ya wanawake wa Uislamu.

### 1.2 Malaengo ya Utafiti

Makala hii imeongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:

1) Kubainisha mihimili itokanayo na matapo tofauti ya nadharia za Ufemenisti kuhusu mwanamke.
2) Kufafanua jinsi mihimili ya matapo tofauti ya nadharia za Ufeministi yanavyoakisi mwanawake.
3) Kutathmini ufaafu wa mihimili ya nadharia za Ufeministi kulingana na mtazamo wa dini ya Uisilamu kuhusu ukombozi wa mwanamke.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

*Corresponding author:
E-mail addresses: jab.alzark@sebhau.edu.ly

*Article History : Received 03 May 2024 - Received in revised form 18 September 2024 - Accepted 30 September 2024*

1) Je, ni mihimili gani itokanayo na matapo ya nadharia za Ufemenisti kuhusu mwanamke?
2) Je, mihimili ya matapo tofauti ya nadharia za Ufeministi yana akisije mwanamke?
3) Je, kuna ufaafu wa mihimili ya nadharia za Ufeminsiti kulingana na mtazamo wa dini ya Uisilamu kuhusu ukombozi mwanamke?

**1.4 Mbinu za Utafiti**

Utafiti huu ni wa kithamano yaani wa kimaelezo. Mtafiti alitumia mbinu ya maktaba kwa lengo la kudurusu kwa kina masuala ya nadharia za ufmenisti, uana, nafasi ya mwanamke katika jamii na masuala ya mwanamke wa Kiisilamu. Data zilipatikana kutoka katika majarida, tafiti za awali kuhusiana na mada ya utafiti huu, vitabu vya dini kama vile, Qu'ran tukufu, hadthi za mtume Mohammad s.a.w na vitabu vyengine.

Data za msingi za utafiti huu ni hoja za wanafeminsti wa Kimagharibu kuhusu suala zima la unyanyasaji na utetezi wa mwanamke. Data hizi zilichanganuliwa kwa msaada wa Nadharia wa Mkabala wa Kiisilamu ukithibitisha upotoshaji wa hoja hizo za wanafeminsti wa Kimagharibi kwa kutumia aya za Qur;an na Hadithi za Mtume s.a.w.

**2.0Viunzi cha Nadharia**

Utafiti umeongozwa na Nadharia ya Ufeministi na Nadharia wa Mkabala wa Kiisilamu. Nadharia ya Ufeministi ulitumika kuonyesha uhalisia wa maisha ya mwanamke katika jamii zao kupitia matapo mabalimbali ya Ufeministi wa Kiitikadi. Ama Mkabala wa Kiisilamu umetumika katika kulijadili suala hili kwa bainisha aya kutoka Qur;an na Hadithi za mtume s.a.w. Aya na Hadithi hizi zikionyesha utukufu wa mwanamke na kupinga hoja za Ufeministi wa Kimagharibi. Hoja ambazo zinazopotosha jamii kwa jumla juu ya udhalilishaji/ utetezi wa mwanamke hasa katika asasi ya dini ya Kiisilamu.

**2.1 Nadharia ya Ufeministi**

Chaundry akirejelewa na Mhunzi (2001) anasema kwamba, madai ya wanawake kutaka haki sawa na wanaume na uhuru wa kujiamulia kazi na mtindo wa maisha wanayotaka ni jambo linaloendelea katika jamii za kimagharibi kwa zaidi ya miaka mia mbili ilyopita. Harakati hizi zinatokana na mapinduzi ya Marekani 1776 na Ufaransa 1789. Mhunzi anaendelea kueleza kuwa wanawake iliwabidi wajikusanye pamoja katika vyama vya wafanyakazi ili kuendeleza mapambano. Migomo, maandamano na uhamasishaji vilisababisha wanaharakati hawa kushambuliwa hata kufungwa. Anaendelea kufafanua kuwa leo hii mwanamke wa kimagharibi amepata baadhi za haki katika siasa, sheria, uchumi na jamii. Hata hivyo mwanamke wa kimagharibi amepoteza usimamizi wake wa familia, utulivu wa akili, heshima na hadhi ya kuwa kwake mwanamke. Maelezo ya Chaundry yanabainisha kuwa msingi wa nadharia ya kifeministi ni harakati zilizoendeshwa na wanawake wa nchi za magharibi.

Khatib (2014) anaeleza kuwa Ufeministi una historia ndefu duniani ulioibua vuguvugu la kutaka kufuta kabisa uonevu wa mwanamke. Chimbuko la ukandamizaji wa mwanamke linatokana na uroho pia tamaa ya mwanaume ya kumdhibiti na kumtawala mwanamke. Agenda kubwa ya nadharia hii ni kumaliza utawala na umwamba wa mwanaume juu ya mwanamke.

Taasisi za kiutamaduni ndizo zinazoshutumiwa kuliendeleza suala hili la ukandamizwaji wa wanawake. Khatib (2014:9) akimnukuu Andrew Dworkin (1976 na 1982:61-62) anaeleza kuwa,

"Ili kufanikiwa, tunahitaji kubomoa kabisa muundo wa mihimili ya utamaduni wa jamii kama vile sanaa, kanisa, sheria, kaya zinazodhibitiwa na baba, jamii na taswira zote za asasi, mila, desturi, ambazo zinamuona mwanamke kuwa mtu ovyo".

Ingawa Dworkin amependekeza njia ya kumkomboa mwanamke, hata hivyo kuna mambo ambayo yanaweza kuonekana kuwa ni ukandamizwaji wa mwanamke katika jamii moja halafu yasiwe ukandamizwaji wa mwanamke katika jamii nyingine. Hali hii inatokana na mpishano wa kiutamaduni iliopo duniani. Dini hubeba dhima kubwa ya kusababisha mipishano hii ya kiutamaduni kati ya jamii moja na jamii nyingine.

Momanyi (2002) naye anatoa tahadhari kuwa, pengine suala la uana na mapambano ya kiitikadi dhidi ya ukandamizwaji wa wanawake halijapokewa vema miongoni mwa jamii za Kiafrika kutokana na dhana kuwa harakati hizo zinatoka Magharibi. Mtazamo wa Momanyi kuhusu nadharia ya Ufeminisiti ni kuwa, ulipingwa katika baadhi ya jamii hasa za Kiafrika. Momanyi anahitimisha kuwa udunishwaji wa wanawake hutofautiana miongoni mwa mataifa. Hitimisho la Momanyi linabainisha kuwa, ingawa wanaharakati wa Ufeministi wanaamini kuwa wanawake kote ulimwenguni wanakabiliwa na mikandamizo ya wanaume hata hivyo wanawake hutofautiana

kimatatizo. Asasi za kiutamaduni hutofautiana kati ya jamii moja na nyingine kutokana na mila, desturi na itikadi zinazoongoza maisha ya jamii husika.

Matapo tofauti ya nadharia hii yameibuka kutokana na kuwepo kwa tofauti ya mikandamizo inayowakumba wanawake kote ulimwenguni. Kutokana na mjadala wa makala hii, matapo ya Ufeministi wa kiitikadi ndiyo yatakayotumiwa kuuendeleza.

**2.2 Nadharia wa Mkabala wa Kiisilamu**

Uisilamu ni dini ya Allah (S.W). Ni mkusanyiko wa kanuni wa maisha ya ambao Allah (S.W) ameutoa kwa ajili ya kumuongoza mwanadamu katika njia iliyonyooka. Uisilamu ni mfumo kamili wa maisha ya mwanadamu.

Makala hii imeongozwa na Mkabala wa Kiislamu. Mkabala wa Uisilamu unatokana na mafundisho yaliyomo katika Qur'ana Tukufu na Hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W). (Taib, 2004). Mkabala wa Kiisilamu unasisitiza mafundisho ya dini ya Uislamu ambayo yanagawanywa kaika sehemu nne kuu. Nazo ni:

i. Nguzo za Uisilamu
ii. Nguzo za Imani
iii. Nguzo za Ihsani
iv. Maadili na sharia ya dini ya Uisilamu

Uchanganuzi wa Makala hii ulijikita katika muhimili wanne ambao ni Maadili na sharia ya dini ya Kiisilamu. Haya ni mambo yale yote yaliyomo na yanatajwa katika Qur'an Tukufu, Hadithi za Mtume (S.A.W), kauli za Makhalifa Rashidun wanne (Abubakar, Omar, Uthman na Ali – RadhiaAllahu Anhum) na kauli za wanachuoni waliobobea katika mafundisho ya dini ambao msingi ni kuamrisha mema na kukataza maovu.

Vile vile muhimili huu ulisaidia kutubainishia aya kutoka Qur'an tukufu na hadithi za mtume s.a.w zinazopingana na Ufeministi wa Kiitikadi.

**3.0 Yaliyoandikwa kuhusiana Matapo ya Ufeministi wa Kiitikadi na Ufeministi wa Kiisilamu**

Haya ni mapitio yaliyoandikwa na watalamu na wanafalsa mbalimbali wakitoa hoja zao kuhusu ukandamizwaji, unywanyasaji, utezi na ukombozi wa mwanamke. Madai yao makuu yamekuwa yakinyoshea vidole asasi za ndoa, kitamaduni na hasa dini. Yfuatayo ni maelezo kuhusiana na hayo.

**3.1 Matapo ya Ufeministi wa Kiitikadi**

Wafula na Njogu (2007) wanabainisha mitazamo mitatu ya Ufeministi kama walivyowanukuu Adamson na wenziwe (1988). Matapo hayo yamebainishwa hapa chini katika sehemu inayofuata;

**3.1.1 Ufeministi Huru**

Wafula na Njogu (2007) wanaeleza kuwa mtazamo huu hutetea usawa kati ya wanaume na wanawake katika ngazi zote za maisha. Kwani binadamu wote ni sawa kwa hivyo wanapaswa kuwa huru. Kwa ujumla tapo hili linatilia mkazo usawa katika mambo yote yanayowahusu wanaume na wanawake. Kusiwepo na upendeleo wa aina yoyote kwani wote wana hadhi sawa.

**3.1.2 Ufeministi wa Kiharakati**

Wafula na Njogu (2007) wanafafanua kuwa wanaharakati wanaoshikilia mtazamo huu wanadai kuwa mwanaume ni adui mkubwa zaidi wa mwanamke. Uwezo wa mwanamke kuzaa ndiyo ambao hutumiwa kumdhalilisha na kutawala mwili wake. Msimamo mkuu wa waitifaki wa mkondo huu ni kwamba, wanawake ni lazima wajitawale wenyewe na washirikiane wao kwa wao hata kimapenzi. Tapo hili kwa ujumla wanaamini kuwa mwanaume hawezi kushiriki kabisa katika suala la kumkomboa mwanamke.

**3.1.3 Ufeministi Kijamaa**

Wakiendelea kufafanua Wafula na Njogu (washatajwa), mkondo huu unahimiza mashirikiano kati ya mwanaume na mwanamke hasa katika majukumu ambayo kimapokeo yalitambuliwa kwamba hufanywa na wanawake. Wanaume wanahimizwa kushiriki kikamilifu katika malezi ya watoto na kadhiya nyingine.

Japo wanawake wanaonekana kukandamizwa, ipo haja ya

kuzichunguza itikadi hizi kama zinaweza kuendeleza mapambano katika jamii zote bila kupingana na itikadi za dini za jamii husika. Inaonekana dhahiri kuwa tapo hili halikuzingatia suala la dini ambazo huwa ndiyo muongozo wa maisha ya jamii husika. Zipo dini ambazo zinatoa muongozo wa kisheria kuhusu majukumu ya wanawake na wanaume. Aidha Mamonyi (keshatajwa) anasisitiza kuwa, ingawa jamii nyingi barani Afrika ni za kuumeni, dhana ya "mwanamke" haikusimamiwa tu na umbo lake au hali za kijinsia. Kwa hivyo, tunapotumia nadharia na mitazamo kutoka nje ya bara hili, tusidiriki kuing'oa mizizi uasili wetu. Msisitizo wa Momanyi ni kuwa, nadharia za kimagharibi zinaweza zisimtendee haki mwanamke anayeongozwa na sheria za kitamaduni. Kwa vile dini ni kipengele muhimu cha kiutamaduni, huweza kusababisha kuwepo na mpishano wa usawiri wa mwanamke kati fasihi ya jamii moja na nyingine.

**4 Ufeministi wa Kiislamu**

Hili ni tapo mojawapo ndani ya ufeministi. Ingawa nadharia hii ni kongwe hata hivyo kujulikana kwake kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na utawala wa kikoloni uliokuwepo katika jamii za kiislamu. Mwaka 1890 utawala wa Muingereza huko Misri uliwalazamisha wanawake wa kiislamu kufuata utamaduni wa kimagharibi ambao unaenda kinyume na Uislamu hasa katika ndoa, malezi, mirathi hata mavazi.

Chaundry (keshatajwa) anaeleza kuwa, mwanamke wa Kiislamu hakulazimika kupambana na kudai haki zake. Hakuanzisha vyama au harakati zozote wala hakufanya madai yoyote ya kutaka haki zake. Uislamu umempa mwanamke wa kiislamu haki nyingi. Haki hizi zote amepewa zaidi ya miaka 1400 iliyopita wakati ustaarabu wa sasa ulikuwa bado hata kumfikiria mwanamke kuwa ni mwanaadamu. Shutuma nzito na kejeli zisizo na msingi zinafanywa na wasomi wasiokuwa Waislamu dhidi ya Uislamu juu ya kutomfanyia haki mwanamke katika mambo ya urithi, elimu, ajira na kushiriki katika masuala mbalimbali ya jamii.

Maelezo ya Chaundry yanabainisha kuwa mwanamke wa Kiislamu hakulazimika kuingia katika mapambano kwa sababu hakukuwa na haja ya kudai haki hizo kwa kuwa tayari zipo na zinaeleweka kishariya. Masuala ya ajira, mirathi, elimu, siasa na mambo mengine ya jamii yameshajadiliwa na kuwekewa ufafanuzi wake.

Muhimili mkuu wa nadharia hii ni kumcha Mwenyezi Mungu kwa kufuata maamrisho yake, yanayotokana na Kurani na hadithi za Mtume (SAW). Kwa ujumla muhimili huu unaegemea kuamrisha mema na kukataza maovu. Aidha nadharia ya mkabala wa Kiislamu ambayo waasisi wake ni Sengo, Ngozi na Taib (2005) nayo ina mhimili huu. Sengo (2009) anasisitiza kuwa binaadamu wameumbwa na Mwenyezi Mungu na wanatakiwa wamtii yeye na Mtume. Kwa hivyo mambo yote yanayofungamana na binaadamu ni lazima yafuate maamrisho yake. Mwandishi, mtunzi na mhakiki wafuate mkondo huu.

Vipengele vya kimsingi vinavyoshughulikiwa na Ufeministi wa Kiislamu kwa mujibu wa Noordin akimnukuu Al-Faruk (2003) viko vitano:

- Mfumo mzima wa familia (aila) katika malezi na ndoa.
- Ubinafsi wa mtu dhidi ya jamii.
- Tofauti za kijinsia katika wajibu wa mwanamke.
- Hadhi ya mwanamke kisheria.
- Suala la ukewenza.

Kwa kuwa suala la umiliki wa mali ni miongoni mwa madai yanayolalamikiwa na wanaharakati wa Ufeministi, makala inaona ipo haja ya kuongeza kipengele cha sita ambacho ni 'haki ya mwanamke kurithi kisheria'.

**5.0 Uchanganuzi wa Baadhi ya Aya na Hadithi zinazopingana na Ufeministi wa Kiitikadi**

Wamitila (2002) anaeleza kuwa dini inatilia mkazo au nguvu itikadi ya kiume inayopatikana katika jamii nyingi. Asasi hii inaishia kuzipa nguvu mpya tamaduni dhalili dhidi ya mwanamke kwa kuziwekea mihimili ya matamko ya kidini.

Zipo aya kadhaa katika Kurani na kutiliwa mkazo na hadithi za Mtume (SAW) ambazo zinazungumzia masuala ya ndoa na hadhi ya mwanamke katika ndoa. Hata hivyo aya hizi hudhaniwa zinamkandamiza mwanamke kwa kuwa zinapingana na itikadi ya ufeministi.

Allah amesema:

*"Wanaume (wawe) ni walinzi wa wanawake kwa sababu Allah amewafadhilisha*
*Baadhi yao kuliko wengine kwa sababu ya mali zao wanazozitoa. Basi wanawake*
*wema ni wale wenye kutii, wanaojihifadhi (hata) wasipokuwepo (waume) zao*
*kwa kuwa Allah amewaamrisha wajihifadhi...*"(4:34)

Imesimuliwa na Abdullah bin Umar (R.A) Mtume (SAW) amesema:

*"Lau ningaliamuru yeyote kumsujudia yeyoye ningaliamuru mke amsujudie*
*mumewe." Tirmidhy (sahihi) hadithi hii ni sahihi.*

Aya na hadithi hii zinapingana na ufeministi. Kwa kuwa ufeministi unasisitiza usawa kati mwanamke na mwanaume lakini matamko haya yanadhaniwa kuwa yamempa haki zaidi mwanaume. Inaonekana wazi kupitia aya hizi mwanamke ataendelea kuwa kifungoni chini ya himaya ya mwanaume. Jambo hili ndilo linalopigwa vita na wanaharakati wa ufeministi huru. Wao wanamini kuwa binaadamu wote ni sawa hivyo kusiwe na ubaguzi wa kumuweka mwanamke chini ya himaya ya mwanaume.

Suala hili limezua migongano ya kiuhakiki wa kazi za fasihi zilizoandikwa na waislamu, hasa zile zenye muelekeo wa kimawaidha. *Utenzi wa Mwanakupona* umekumbwa na kadhiya hii. Kwa mfano Sengo (2009) anafafanua kuwa mama ampamba bintiye awe mke shani, mwenye kujipamba na kupendeza na kuwa mke bora. Anahoji kuwa ni nani asiyetaka kuwa mke bora? Ila kwa mabinti wanaoyakana ya Mwenyezi Mungu na ya Mtume (SAW) na wenye kubishana na wazazi wao. Muelekeo wa uhakiki wa Sengo unatokana na kuongozwa na nadharia ya Uislamu. Khatib (2014) ameongozwa na Ufeministi wenye msingi wa kimagharibi. Anaona kuwa mtunzi anamfunga bintiye kitanzi cha utumwa na kumtaka aolewapo asiwe mke mwenye kutaka haki sawa mbele ya mume bali awe mtumwa wa mume. Ndoa hapo inakuwa taasisi ya ukandamizwaji wa mwanamke.

Kwa kuwa Khatib (amekwishatajwa) anakiri kuwa ndoa ni taasisi. Anaendelea kudai kuwa ili taasisi iweze kudumu na kusonga mbele kimaendeleo ni lazima iwe na uongozi imara na wenye mshikamano. Mwenyezi Mungu kumuinua mwanaume na kuwa msimamizi wa mwanamke hakumnyang'anyi mwanamke uhuru wake. Bali kunastawisha maelewano ikiwa wote ni waelewa. Mwanaume kimajukumu yeye ndiye mkimu wa familia ingawa uislamu haumkatazi mwanamke kulitekeleza hili, hali ikiruhusu.

Suala la utoaji wa mahari wanaharakati wengi wanaamini kwa namna moja linamnyanyasa mwanamke. Kwani wanaume walio wengi huona wameuziwa bidhaa, kwa hivyo waitumie watakavyo. Hata hivyo ni suala la ajabu ya kuwa mtu kuhalalishiwa kifaa lakini ukashindwa kukienzi. Je, inafaa kukitumia vibaya ili kiharibike? Wanaharakati wa upande wa Ufeministi wa kiharakati wakatoa msimamo kuwa wanawake wajitawale wenyewe kwa wenyewe na washirikiane wao kwa wao hata kimapenzi.

Zipo kazi kadhaa za fasihi ambazo zimesawiri hali hii. Wahusika kama vile wake wa Madahiro katika *Machozi ya Mwanamke* (1977) na Mwamvita katika *MaaEe* (1987) ni wanawake waliogeuzwa watumwa katika ndoa kwa kisingizio cha mahari. Mbali ya kutumikishwa wanawake hawa wamekuwa wakipigwa na waume wao kadiri wanavyojisikia.

Hata hivyo uisilamu unaichukulia mahari kama zawadi tu anayopewa mwanamke. Wala Uislamu haukuweka kima maalumu wala mali maalumu ambazo zingetolewa kama mahari. Kwa hivyo suala la mahari ni makubaliano baina ya mke na mume. Na wala siyo nguzo ya dini ya uislamu kama ilivyo kwa utoaji wa zaka.

Vile vile Mtume (SAW) anasema,

"*Naapa kwa ambae nafsi yangu imo mkononi mwake! Mwanaume yeyote anemwita*
*Mkewe kitandani mwake naye (mke ) akamkatalia, kwa hakika alie mbinguni*
*Humkasirikiya mwanamke huyo mpaka mumewe amuwekee radhi.* "(Abuu Huraira)

Abuu Huraira (RA) amesema Mtume (SAW):

*"Mwanamume atakapomwita mkewe kitandani (ili alale nae) akakataa ,akalala (mume*
*huyo)akiwa amemkasirikia (mkewe), malaika watamlaani (mke huyo) mpaka*

*apambaukiwe*". (Muttafaq Alayhi)

Hadithi hizi za mtume zinamuhimiza mwanamke kuwa awe tayari wakati wowote kumstarehesha mumewe. Pindi mwanamke anapokataa huwa anapata laana. Jambo hili linakemewa vikali na wafeministi wa kiharakati, wanadai uwezo wa mwanamke kuzaa ndiyo unaosababisha kuingia matesoni. Kwa hivyo hadithi hizi zinapingana na tapo hili.

Watunzi kadhaa wameshutumiwa na wahakiki kwa kuwachora wanawake kama 'pambo' au 'chombo cha starehe'. Kwa mfano Khatib (keshatajwa) akiushambulia *Utenzi wa Mwana Kupona* kwa kumkweza mwanamume na kumdunisha mwanamke anadai kuwa, ili kumtisha mwanawe mama anamwambia kuwa uwezo wa radhi za mume kwa mke ndizo zenye uwezo wa mwisho. Hata siku ya kiyama ataweza kuamua kuwa mke aende peponi au motoni. Tazama beti hizi hapa chini;

26 *Siku ufufuliwao*
*Nadhari ni ya mumeo*
*Taulizwa atakalo*
*Ndilo takalotendewa*

27 *Kipenda wende peponi*
*Utakwenda dalhini*
*Kinena wende motoni*
*Huna budi utatiwa*

Khatib anasema, uwezo wa kwenda peponi au motoni ni hatma ya mume wa mtu. Madaraka hayo ni makubwa mno. Uonevu ulioje umwandamao mwanamke? Baada ya kitisho hicho ambacho si kidogo, mama mzazi anamuusia mwanawe yale yaliyomlazimu kuyafanya kwa kumstarehesha mume.

Inaelekea wazi mhakiki huyu hakuutendea haki *Utenzi wa Mwanakupona*, kwani mtunzi aliegemea kwenye mafundisho ya hadithi za Mtume (SAW) na kuutumia utenzi huu kama mawaidha kwa mwanawe. Beti za (26 na 27) zipo chini ya mwongozo wa hadithi zinazomhimiza mke kumridhia mume ili Mwenyezi Mungu awe radhi naye.

Suala la mwanamke kuonekana mtumwa limesawiriwa vya kutosha katika kazi mbalimbali za fasihi. Tamthilia ya *Machozi ya Mwanamke* na *Mama Ee* zimesawiri vilivyo kipengele cha ndoa zenye muelekeo wa mapambano yanayopigiwa debe na Ufeministi. Muhusika Mwavita katika tamthilia ya *Mama Ee* anaonekana kuvalia njuga harakati za Ufeministi.

MWAVITA: *Wajua mama, wake wataendelea kunyonywa na kunyanyaswa*
*na mabwana kwa kutojua haki zao . Wengi washakubali kuwa*
*wananchi wa tabaka la chini! Ati ndiyo Mungu alivyotuumba.*
*Wake kama hao huwachukuwa waume kama Mungu.*
*Mtu kama mimi huchukuliwa kama mwasi.*
*Nimeasi dini gani? Kuabudu*
*Waume (kwa hasira)...! Simwabudu mume yeyote!* (Uk.59)

Ujumbe alioubeba Mwavita ni kuwalaumu wanawake wote wanaowanyenyekea waume zao. Hali hii anaiona inaendeleza unyanyasaji wa mwanamke. Mwavita anaendelea kukishitumu kipengele cha dini ambacho humhukumu mwanamke anayekimbia manyanyaso ya mume kuwa ni uasi. Hata hivyo uislamu haukumshurutisha mwanamke kuyatii mambo ambayo yapo kinyume na mamrisho ya Mwenyezi Mungu.

Vile vile mwanaume wa kiislamu ameruhusiwa kuoa wake wawili, watatu, wanne au mmoja. Mwenyezi Mungu anasema katika Kurani tukufu:

*"...Oeni mnaowapenda kati ya wanawake wawili,watatu,wanne na mkihofia kufanya*
*uadilifu oeni mmoja*".(4:2)

Uke wenza ni jambo linalojadiliwa sana na wanaharakati wa kifeministi wanaodhani Uislamu unamdhalilisha mwanamke. Kwa kuwa mwanaume amepewa ruhusa kisheria ya kuoa mke zaidi ya mmoja, aya hii inapingana kabisa na ufeministi huru ambao unapigania usawa kati ya mwanamke na mwanaume. Hapa hudhaniwa dini imempendelea mwanaume.

Mwaka 1988 nchini Tanzania yalifanyika maandamano makubwa katika kisiwa cha Unguja kuipinga kauli ya Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake nchini Tanzania kwa wakati huo, marehemu Safia Kawawa. Mwenyekiti huyu alitaka wanawake nao wapate haki ya kuolewa na mume zaidi ya mmoja.

Watunzi wa kazi za fasihi wamekuwa wakilisawiri suala hili hasa kwa kuonesha yale matatizo yanayowakumba wanawake waliomo katika ndoa za aina hii. Wanawake wamekuwa wakinyanyasika kwa namna moja au nyingine katika suala hili. Hili linatokana na baadhi ya wanaume kuegemea upande mmoja na kumtelekeza mke wa pili (na kinyume chake) pamoja na watoto. Hali hii inawasilishwa vema katika riwaya ya *Kiza katika Nuru* ya Khamis na *Barua Ndefu Kama Hii* ya Mariama Ba. Kama inavyojidhihirisha katika barua iliyoandikwa na Ramatulay kumpelekea Dauda Dieng:

*"Suala la mitala wewe waliona japesi.Wale wanaojiingiza katika suala hili wanajua vikwazo vyake uwongo wake na dhuluma, mambo ambayo huifannya mioyo yao iwe mizito kutokana na furaha ya muda mfupi isababishwayo na tamaa ya kufanya mabadiliko kwamba mapenzi ndiyo kihamasisho chako, na yamekuwepo hata kabla hujaoa na wala majaaliwa hayajaridhisha kikunjufu. Isitoshe kuwepo kwa mke na wanao kunaifanya hali itatanishe zaidi. Mimi ambae hivi majuzi tu nilitelekezwa kutokana na mbinu za mwanamke. Nisingeweza kujiingiza haraka haraka kati yako na familia yako..."(Uk.92)*

Kumekua na pingamizi hapa na pale katika utekelezaji wa ruhusa hii. Wanawake walio wengi wanalipinga suala hili. Hii ni kutokana na kuchelea kukumbwa na matatizo ambayo yamewakumba wanawake wenzao waliotangulia. Vipingamizi hivi vinasababisha wanaume kuoa kwa siri. Hali hii katika jamii ipo kwa wingi na hata wasanii wamelibainisha kupitia katika nyanja ya fasihi. Riwaya za Abdulla za *Duniani Kuna Watu* (1973) na *Kosa la Bwana Msa* (1984) zinaonesha kadhiya hii na athari zake. Ndugu wa baba mmoja Saleh na Seluma wanaoana, tena kutokana na ushauri wa baba yao katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu* kama inavyobainishwa na mwandishi:

"*...alijibu Bwana Hakim...Hadi ni jambo la kupendeza na kufurahisha. Kwa mimi*
*nafsi yangu, nakuomba Selume, naona hapana mume wa kukufaa ila Saleh na*
*kadhalika Saleh sioni mke wa kukufaa wewe unasemaje bwana Saleh?"*(Uk.30)

Saleh (2011:72) anaeleza kuwa, "Kwa vile ndoa ni mpango aliouandaa Mwenyezi Mungu kwa viumbe wake, hautakosa taratibu zake ambazo kama hazikufuatwa na wanandoa, ndoa hiyo itakuwa na kasoro." Kwa ujumla maelezo ya Saleh yanabainisha kuwa ukiukaji wa sheria za ndoa husababisha matatizo katika familia.

Issa (2011) anatoa ufafanuzi ufuatao kuhusu uke wenza, anaeleza kuwa suala jengine linalohusiana na ndoa ni suala la uke wenza. Katika kazi za Mohamed Said Abdulla, tunaona kwamba ukewenza ni suala zito kwa wanawake. Bi. Shena mama yake Selume anamlazimisha mumewe Hakimu Marijani kumwacha mke mdogo Bi. Mariyamu Mkembe. Kwa vile hawezi joto la uke wenza. Naye Bi. Shinuna anampinga mumewe kwa kumuoa Jamila ambaye ni mke mdogo. Tunaona mwishowe Bi. Shinuna anapanga mpango wa kumuua mumewe kutokana na kukaidi kwake suala la kuacha kwenda Chwaka kwa Jamila.

Uhakiki wa Issa kuhusu taswira ya mwanamke katika riwaya za Mohamed Said Abdulla, unatoa taswira kamili la suala la ukewenza. Hata hivyo suala la uke wenza limeruhusiwa katika Uislamu kwa hekma maalumu, ikiwemo mke kuwa mgonjwa na idadi kubwa ya wanawake ukilinganisha na wanaume. Aidha suala hili halikulazimishwa kisheria bali limewekewa sharti la uadilifu.

Katika Uislamu talaka ni halali ingawa ni katika hali inayomchukiza Mwenyezi Mungu lakini bado wanandoa wanaruhusiwa kuachana hasa ikiwa suluhu imeshindikana. Kwa hivyo Uislamu haukumtia kifungoni mwanamke. Suala la kujadiliwa ni wanaume kama kweli wanaoa kwa kufuata maandiko ya dini au wanaongozwa na utashi wao. Zipo aya na hadithi za Mtume ambazo zinawataka wanaume kuwafanyia mema wanawake.

Mwenyezi Mungu anasema:

*"Nanyi hamuwezi kufanya uadilifu (kweli kweli) baina ya wake, ijapokuwa*

*mtataka kufanya kufanya hivyo. Kwa hivyo msielekee (upande mmoja)*
*kabisa kabisa, msije kumwacha (huyo mwengine msiyempenda) kama*
*aliyeangukwa, anasukumika huku na huku;hajijuwi kuwa ana mume ama*
*mjane. Na mkisulihishana (sasa) na kumcha Allah. Basi Allah ni mwingi wa*
*msamaha na mwingi wa rehema."* (4:129)

Abuu Huraira (RA) amesema "Mtume (SAW)"
*"Wafanyieni kheri wanawake, hakika mwanamke ameumbwa kwa ubavu' na*
*Hakika sehemu iliyopotoka zaidi katika ubavu ni ile ya juu, ukitaka kuunyoosha*
*Utauvunja na ukiuwacha utaendelea kupotoka, kwa hivyo wafanyiyeni wema*
*wanawake."* Muttafak

Almughira bin Shu'bah (RA) amesimulia: Mtume (SAW) amesema, "*Hakika Allah amewaharamishia kuwaasi akina mama, kuzuia mali kwa ubakhili*
*Na kuyakusanya kwa pupa, kuwazika mabinti. Na amechukia kwenu maneno ya*
*Uvumi, kuuliza sana na kuharibu mali*." Muttafak Alayhi.

Kwa ujumla nukuu hizi zinawahimiza wanaume kuwatendea kheri na kushirikiana na wanawake. Pia mwanamke anaokolewa kidini kutoka vitendo vya kidhalimu ambavyo alikuwa akitendewa wakati wa kipindi cha ujahili. Ilhali ufeministi wa kiharakati unapinga kabisa mashirikiano kati ya viumbe hawa. Kwani wanaharakati hawa wanaamini adui mkubwa wa mwanamke ni mwanaume, kwa hivyo wanawasisitiza wanawake wasishirikiane kabisa na wanaume.

Suala la umiliki wa mali na urithi limewekwa kwa kufuata muongozo wa Kurani tukufu. Hata hivyo nalo limejengewa hoja na wanaharakati wa ufeministi. Chaundry (keshatajwa) anaeleza kuwa katika sheria ya Kiyahudi, mabinti na wamama walibaguliwa katika urithi. Mabinti wa Kibaniani na Wahindi walibaguliwa katika urithi. Waliokuwa na haki ya kurithi ni watoto wa kiume tu. Kwa mara ya kwanza mwanamke amepata haki ya kurithi baada ya kushushwa sura ya nne ya Kurani. Chaundry anafafanua kuwa:

*"Imepokewa katika hadithi sahihi kwamba sahaba mmoja wa Bwana Mtume (SAW)*
*Alifariki katika vita vya Uhud na akaacha mjane na mabinti wawili. Familia hii ilikuwa*
*Tajiri lakini baada ya kifo cha kiongozi wa familia, ndugu yake akachukua mali kwa*
*mujibu wa mila za kipagani na hakuacha chochote kwa ajili ya mjane na mabinti*
*mayatima. Katika hali hii ya kuhuzunisha, mjane yule pamoja na mabinti zake*
*walimwendea Bwana Mtume (SAW) na kumfahamisha hali hiyo.*" (20)

Kutokana na kisa hiki ndiyo sharia ya mirathi iliyomo katika sura ya nne ikaanza kutumika na kwa mara ya kwanza binti na mjane wakaanza kurithi.

Mwenyezi Mungu anasema:
*"Wanaume wana sehemu katika mali wanayowaachia wazazi na jamaa waliokaribia.*
*Na wanawake pia wanayo sehemu katika yale waliyoyaacha wazazi na jamaa*
*Waliokaribia yakiwa kidogo au mingi." (4:7)*

*"...Mwenyezi Mungu anakuusieni juu ya watoto wenu mwanaume apate sawa na sehemu*
*Ya wanawake wawili..." (4:11)*

Aya hizi kwa Ufeministi huru hudhaniwa kuwa zinamkandamiza mwanamke. Kwa kuwa binadamu wote ni sawa, hakuna haja ya kuwepo mpishano wa kiurithi kwa kuwa wote wana hadhi sawa ya kuwa watoto.

Hata hivyo Uislamu ndiyo uliompa mwanamke haki ya kurithi. Kimajukumu, mwanaume analazimika kuitafutia maisha familia ilhali mwanamke ahusiki na hili. Aidha Uislamu unahimiza malezi ya kifamilia ambapo mwanamke anakua chini ya uangalizi wa mwanaume. Anapokuwa mtoto anakuwa chini ya uangalizi wa baba. Anapofariki baba, kaka hutakiwa kuchukua jukumu hili au babu au baba mdogo. Mwanamke anapoolewa anakuwa chini ya uangalizi wa mume.

Uislamu haumnyimi mwanamke haki ya kumiliki mali. Mwenyezi Mungu anasema:
*"...Na wanawake nao wanayo sehemu (kamili) ya vile walivyyovichuma".(4:32)*

Ingawa mwanaume ana majukumu ya kuikimu familia hata hivyo uislamu haikumnyang'anya mwanamke haki yake ya kumiliki mali kama ilivyo kwa mwanaume. Hali mwanamke kutomiliki rasilimali yoyote imesawiriwa vilivyo katika fasihi. Kwa mfano Khatib (2003) katika shairi la "Mwanamke",

*Namuona yu shambani,*
*Na jembe mikononi,*
*Mwanamama,*
*Mavuno si yake,*
*Ni ya mumewe*
*Kwa nini mwanamke,*
*Ni yeye peke yake,*
*Anyimwaye,*
*Heshimaye,*
*Haki anakosa,*
*Kwa kweli ni kosa. (16 )*

Khatib katika beti hizi anaonesha hali ya mwanamke katika ndoa, kuwa ni kiumbe mwenye kujituma katika kazi. Ingawa mwanamke ndiye anayefanya kazi lakini pato lote ni mali ya mumewe. Kwa kuwa mwanaume ndiye mmiliki wa mke na pato la mke pia humstahikia mume.

Hali ya mwanamke kunyang'anywa mali imechochea kwa kiasi kikubwa wanawake kutaka kujinasua na kusababisha ugomvi katika ndoa. Hali hii inajitokeza katika tamthilia ya *Machozi ya Mwanamke.* Wake wa Madahiro wanagoma kuondoka nyumbani kwa Madahiro bila ya kugawana mali ambayo waliichuma pamoja. Jambo hili linapingwa vikali na Madahiro na kuwashangaza wengine wenye mtazamo sawa na Madahiro. Hali kama hii inajitokeza pia katika tamthilia ya *Mama Ee.*

KINAYA:*...wanawake wenzako hawazioni ingawa wafanyakazi wapewa na mabwana zao za kutosha kununua chakula tu. Zilobaki zote afutika bwana maana aliilipa Mahari...Mwanamke hana chake. Akisha olewa kila kitu hata yeye mwenyewe ni mali ya bwanake. Ndiyo sheriya ya kikwetu wacha uzungu hapa."(*Uk.14*)*

Ingawa muhusika Kinaya analalama kuwa suala la umiliki wa mali ni la kizungu lakini Uislamu umeshayafafanua haya tangu zamani.

Kwa ujumla dini ya kiislamu inapingana kwa kiasi kikubwa na nadharia ya ufeministi juu ya mwanamke. Kwa kuwa kipengele cha nafasi ya mwanamke kimekuwa muhimu katika kuzihakiki kazi za fasihi, kunaweza kuzua mpishano wa kiuhakiki. Linaloshituwa zaidi ni kuwa kazi za fasihi hutungwa kwa kuegemea zaidi kipengele cha utamaduni wa jamii husika, bali kazi hizi huhakikiwa kwa kutumia nadharia zenye msigi wa utamaduni wa jamii nyingine tofauti na ile iliyokusudiwa katika kazi husika.

**6.0 Hitimisho**

Kwa mujibu wa hoja zilizojadiliwa, ipo haja kwa wahakiki kutumia nadharia inayofaa kulingana na utamaduni ulioizaa kazi ya fasihi husika. Hoja zilizojadiliwa zinaonesha bayana kuwa si kila nadharia huweza kutumika kama dira ya kuongoza tahakiki na tafiti za fasihi. Kuna haja ya kuyachunguza vema matatizo yanayowahusu wanawake kwa kuegemea vipengele vya utamaduni wa jamii husika. Dini ni kipengele kikuu kinachotoa muelekeo wa vipengele vyengine vya utamaduni. Kwa maneno mengine itikadi, mila na desturi huathiriwa kwa kiasi kikubwa na imani ya dini ya jamii husika. Kwa hivyo mhakiki au mtafiti ili aweze kuitendea haki kazi ya fasihi, mtunzi na hata hadhira aliyoilenga ni vema kuzingatia utamaduni wa jamii husika.

**Marejeo**

[1]- Abdulla, M.S.(1973). *Duniani Kuna Watu*. Dar es salaa :East African Publishing House. *(1984). Kosa la Bwana Msa*. Nairobi :Aeme Press Ltd ..

[2]- Ch*anjo Matakwa ya Mwanaume Katika Mwili wa Mwanamke*. Dar-es salaam (2014).

[3]- Chembe, A. H. (2022) "Uathiriano Matini katika Tenzi Mfano wa Utenzi wa Hati na Utenzi wa Mwanakupona katika Ushairi wa Kiswahili" Tasnifu ya Uzamifu (Hijachapishwa) Chuo kikuu cha Pwani.

[4]- Chomboz: *Taswira katika Wasakatonge* 27-6-2013 Chomboz.blogspot .com /2013/04.

[5]- Issa, A. A. (2011). "*Taswira ya Mwanamke katika Riwaya za Muhammed Said Abdulla*". Makala za Kumuenzi Muhammed Said Abdulla. Zanzibar: Chuo Kikuu Cha Elimu Chukwani.

[6]- Ibrahim, U.A na Maguo, M.O (2020) "Mchango Wa Dini ya Kiislamu katika Kujenga Utangamano wa Kimbari katika Jamii ya Zanzibar: Mifano Kutoka Katika Riwaya ya *Vuta N'kuvute*". *Jarida La Chalufakita* 2020, Juzuu Na. 2.

[7]- Khatib, M.S.(2003). *Wasakatonge*. Dar-es salaam: Oxford University Press Limited.Taasisi za Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

[8]- Mhunzi, B.H (2001). *Haki za Wanawake katika Uislamu: Ajira, Mirathi, Elimu na Siasa*. Dar-es salaam: Media Center

[9]- Mariama Ba. (1980) *Barua NdefuKama Hii*. Tanzania. Mkuki na Nyota Publishers.

[10]- Mohammed, S.A.(1988). *Kiza Katika Nuru*. Kenya: Oxford University Press, East Africa Ltd.

[11]- Momanyi, C. (2002). *Utafiti wa Kiswahili na Masuala ya Uana: Suala la Uana Katika Utafiti wa Kiswahili*. Kenya University Press.

[12]- Mwachofi, A.K. (1987) *MamaEe* .Nairobi :Josaphat O. Mithiga.

[13]- Ngozi, I.S. (1977) *Machozi ya Mwanamke*. Dar es salaam: Tanzania Publishing House.

[14]- Noordin, M.M. (2009), "*Ufasiri wa Ufeministi wa Kiislamu katika Utamaduni wa Mwanamke Mswahili: Mkabala au Ushirikiano."* Kenyata University.

[15]- Salim, A.A. (2011) "*Mafunzo na Ujumbe katika Riwaya za Muhammed Said Abdulla*.Makala za Samina za Kumuenzi Muhamed said Abdulla. Zanzibar: Chuo Kikuu cha Elimu Chukwani.

[16]- Sengo, T.S. (2009). *Fasihi za Kinchi*.Dar es salaam: Al Aminand Reserch Academy.

[17]- Sharif, Z.Y. (2009). Tafsiri ; Maalim, U An-*Naway*:*RiyadhulSwalihina*. Mombasa: Kenya.

[18]- Taib Ali, A. H. (2021) "Mafundisho ya Iktibasi katika Utenzi wa Mtu Ni Utu wa Ahmad Nassir Juma Bhalo (Ustadh Bhalo)". *Kioo cha Lugha*, Juz. 19 (1), Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Uk, 128-144.

[19]- Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Kenya: The Jomo Kenyatta Foundation.

[20]- Wandera-Simwa, S. P. (2021) "Mwanamke wa Kiswahili katika Utenzi wa Mwanakupona" *East African Journal of Swahili Studies* Volume: 4 uk, 82-98. (Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.4.1.422

[21]- Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phonix Publishers Ltd.